MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

TAARIFA KWA UMMA

Tareh: 14 Juni, 2018

UFAFANUZI JUU YA USHIRIKISHWAJI WA WAAJIRI KATIKA UANDAAJI MITAALA NA UTOAJI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) inapenda kutoa ufafanuzi juu ya habari iliyoandikwa na Gazeti la Nipashe **katika toleo lake Namba 0579595 la tarehe 11 Juni 2018, ukurasa wa 21, yenye Kichwa cha Habari, "Siri Wahitimu Vyuo Veta Waweze Ajirika."** Maudhui ya habari hiyo ni kuwa **VETA haiwashirikishi waajiri katika uandaaji wa mitaala na utoaji wa mafunzo na kuwa hilo linachangia katika kufanya wahitimu wake wasiajirike**. Habari hiyo ilinukuu mawazo yaliyotolewa na Mratibu wa Ukuzaji Ujuzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) nchini, Bw. Helbert William wakati akizungumza na vijana wanaotekeleza Mradi wa Kuwaendeleza Vijana Wajasiriamali unaoendeshwa na Shirika la Technoserve mkoani Mbeya. Katika habari hiyo, Bw. Helbert William anadaiwa kusema kuwa, "changamoto ya ajira ipo duniani kote, lakini nchini (yaani Tanzania) inatokana zaidi na wanafunzi kufundishwa vitu ambavyo haviendani na mahitaji ya waajiri na kuwa vijana wengi wanasoma wakijiandaa kuajiriwa badala ya kusoma kwa ajili ya kujiajiri."

Mwandishi huyo alimnukuu Bw. Helbert William akisema, "tunataka mabadiliko kwenye utungaji wa mitaala, tunataka waajiri washirikishwe kikamilifu na ikiwezekana wao wenyewe washiriki kwenye ufundishaji wa vijana hao ili vijana wasome wakiwa wanajua mahitaji ya waajiri"

Tunashukuru mawazo ya mdau huyo pamoja na wadau wengine ambao wamekuwa na shauku ya kuona vijana na wananchi wanaohitimu elimu na mafunzo ya ufundi stadi wanapata mafunzo bora na hivyo kuweza kuajirika zaidi na kuchangia katika maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii. **Hata hivyo, tunapenda kutoa ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:**

1. **Mlengo wa VETA katika kutoa na kusimamia mafunzo:** Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1994, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ikiwa ni taasisi iliyopewa dhamana ya kutoa na kusimamia Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini, daima mfumo wake umekuwa ni wa kuzingatia **mahitaji ya soko la ajira.**

2. **Mchakato wa uandaaji mitaala:** Kutokana na VETA kuwa muumini wa mahitaji ya soko la ajira, mchakato wa uandaaji mitaala na utoaji wa mafunzo unatoa kipaumbele katika utafiti wa soko la ajira na ushirikishwaji wa waajiri na wadau wengine. Mchakato hufuata hatua mbalimbali zikiwemo:

   i. **Utafiti wa soko la ajira** ambapo taarifa za hali ya mahitaji ya ujuzi hukusanywa na kutathminiwa kwa utafiti wa kina ukiwashirikisha waajiri, wadau mbalimbali na wananchi kabla ya kuandaa viwango vya mafunzo pamoja na kuanzisha au kurejea mitaala yeyote. Kutokana na kuona umuhimu wa eneo hili, VETA inayo Kurugenzi ya Soko la Ajira, Mipango na Maendeleo ambayo pamoja na mambo mengine husimamia utafiti wa taarifa za soko la ajira. Aidha, katika Kanda zake 9, kila Kanda inaye mtumishi mmoja mahsusi kwa ajili ya utafiti wa soko la ajira (Labour Market Analyst). Taarifa ya soko la ajira hujadiliwa na wadau mbalimbali wakiwemo waajiri kabla ya kurasimishwa na kutumika;

   ii. **Kutafsiri taarifa za soko la ajira na kuandaa rasimu ya mtaala:** Walimu na wataalam wa mafunzo hushirikishwa katika kutafsiri matokeo ya utafiti na kuandaa rasimu ya mtaala;

   iii. **Ushirikishwaji wa waajiri na wataalam katika kuandaa mitaala:** Bodi ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET Board) imeunda Kamati maalum za Wataalam Washauri wa Fani (Trade Advisory Committees-TACs) katika kila sekta ya mafunzo. Kamati hizo zimepewa jukumu la kutoa ushauri katika mchakato wa uandaaji na uboreshaji wa mitaala mbalimbali katika sekta husika za mafunzo. Wajumbe wa kamati hizi huwa ni wataalam wabobezi katika maeneo husika ya mafunzo na ambao wako kwenye soko la ajira-kazini. Hivyo wanao ufahamu mkubwa wa mwenendo wa soko la ajira katika fani zao;

   iv. **Ushirikishwaji wa wadau wengine:** baada ya rasimu ya mtaala kukamilika na kupitishwa kwenye Kamati za Wataalam Washauri wa Fani (TACs), VETA huandaa mikutano ya wadau (Stakeholders Forums) kwa ajili ya kupitia na kutoa maoni yao kwenye rasimu za mitaala;

   v. **Uidhinishaji wa mitaala:** Baada ya kukamilika, mtaala huidhinishwa na Bodi ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Bodi hii inaundwa kwa uwakilishi ikihusisha wawakilishi wa waajiri, wawakilishi wa wafanyakazi (waajiriwa), wawakilishi wa Serikali, na wawakilishi wa Asasi za Kiraia. Kwa hiyo, hata maamuzi ya Bodi katika kuidhinisha mitaala hufanyika kwa ufahamu wa taarifa za hali ya soko la ajira;

   vi. **Utekelezaji wa mtaala na mrejesho:** Baada ya Bodi kupitisha mtaala, utekelezaji wake huanza huku mrejesho kutoka kwa wadau na watumiaji wa mtaala husika ukiendelea kupokelewa;

vii. **Tathmini na mapitio:** Baada ya kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji, mtaala hufanyiwa tathmini na mapitio na kisha uboreshaji kama kuna mabadiliko kulinga na mrejesho kutoka kwa wadau na taarifa za utafiti wa soko la ajira.

3. **Ushirikishwaji wa waajiri katika mafunzo:** VETA imekuwa ikishirikisha sana waajiri katika kutoa mafunzo, huku ikiwa na programu mbalimbali mahsusi za mafunzo kwa kushirikiana na waajiri. Miongoni mwa programu za mafunzo kwa kushirikiana na waajiri ni:

   i. **Mafunzo ya Uanagenzi kwa Kushirikiana na Viwanda/Waajiri (Dual Apprenticeship Training):** Ni mpango unaohusisha mafunzo ya mahali pa kazi na chuoni. Msisitizo mkubwa umewekwa kiwandani kwa kuwa huko ndiko Mwanagenzi (Apprentice) hupata fursa pana ya kufanyia kazi aliyojifunza chuoni. Mpango huu ambao tunauendesha kwa kushirikiana na **taasisi mbili za kijerumani za** Hamburg Chamber of Skilled Craft na Westdeutscher Handwerkskammertag unahusisha mafunzo ya ufundi magari, ufundi umeme, huduma za hoteli na masuala ya uendeshaji na utengenezaji wa zana za kilimo. Tangu kuanza kwa mpango huu mwaka 2013 hadi sasa, makampuni/viwanda (waajiri) zaidi ya 78 wameshiriki katika kutoa mafunzo kwa kushirikiana na VETA.

   ii. **Mafunzo ya Uanagenzi kwa Kushirikiana na Makampuni ya Madini:** Tangu mwaka 2008**,** VETA kupitia chuo chake cha Moshi kwa kushirikiana na Chemba ya Madini na Nishati (TCME) na Makampuni ya Madini inaendesha mpango wa mafunzo ya ufundi stadi kwa ajili ya kuhudumia shughuli za migodini na ujenzi. Programu hii kwa Kiingereza huitwa Integrated Mining Technical Training Programme (IMTT). Katika programu hii, VETA imekuwa ikishirikiana na makampuni ya Bulyanhulu, Buzwagi, North Mara, Geita Gold Mining, Kabanga, Sandvick, Mantra, Pan- Africa, Atlas Copco na Shanta katika kutoa mafunzo ambapo mwanagenzi hutumia muda fulani chuoni na mwingine mahali pa kazi.

   iii. **Mpango wa Kuboresha Ujuzi kwa waajiriwa (SEP):** Katika mpango huu VETA hushirikiana na waajiri katika kuboresha ujuzi wa wafanyakazi ili uendane na mabadiliko ya teknolojia katika fani zao. Katika kipindi cha miaka mitano tangu 2012 hadi 2017 Mpango huu nao umeyashirikisha makampuni 74.

4. **Kuajirika kwa wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi:** VETA hufanya ufuatiliaji wa hali ya wahitimu wake kila baada ya miaka mitano na taarifa zinaonesha kuwa kuhitimu wengi wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi wamekuwa wakiajirika ndani ya miezi sita tangu kuhitimu. Mathalani taarifa za mwisho (2010) zilionesha kuwa asilimia 66.1 ya wahitimu walipata ajira ndani ya miezi sita tangu kuhitimu. Kati hao waliopata ajira ndani ya miezi sita, 50% walikuwa wamejiajiri wenyewe, hali inayodhihirisha kuwa wahitimu wengi hawategemei kuajiriwa, badala yake wanajiandaa kujiajiri.

5. **Kuaminika kwa Mafunzo ya Ufundi Stadi kama Suluhisho la Ajira:** Elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini yamezidi kuaminika kuwa mojawapo ya suluhisho muhimu la ajira nchini. Hali hiyo inadhihirishwa na takwimu za ongezeko la watu wanaoomba kujiunga na mafunzo hayo kila mwaka kutoka katika makundi mbalimbali yenye viwango tofauti vya elimu kama inavyoonekana katika takwimu hapa chini:

Walioomba kujiunga katika vyuo vinavyomilikiwa na VETA

	Darasa la VII	Kidato cha IV	Kidato cha VI	Cheti	Stashahada	Shahada	Shahada ya uzamili
2014	**3174**	**17975**	**61**	**0**	**0**	**0**	**0**
2015	**2373**	**14749**	**42**	**14**	**2**	**1**	**0**
2016	**2212**	**10608**	**42**	**16**	**3**	**2**	**0**
2017	**3583**	**9337**	**315**	**87**	**140**	**113**	**18**
2018	**1498**	**9016**	**64**	**73**	**9**	**4**	**2**
Jumla	**12840**	**61685**	**524**	**190**	**154**	**120**	**20**

Chanzo: Takwimu za maombi ya kujiunga na Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika vyuo vya VETA kama zilivyochambuliwa kutoka katika mfumo wa VETMIS.

HITIMISHO

Licha ya changamoto mbalimbali katika utoaji na usimamizi wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi, mara zote VETA imekuwa ikizingatia umuhimu wa mahitaji ya soko la ajira katika utoaji wa mafunzo na imekuwa ikifanya juhudi za kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo waajiri kwenye kupata taarifa za soko la ajira; uandaaji wa mitaala; utoaji wa mafunzo; pamoja na kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika vyuo mbalimbali vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini yanayowawezesha wahitimu kuajiriwa na kujiajiri.

Imetolewa na:

Dkt. Bwire Ndazi
Kaimu Mkurugenzi Mkuu